TATHMINI YA MTAALA WA UMILISI



GREDI LA SITA

KISWAHILI

MJARABU WA UFUNGUZI WA MUHULA WA 3 2023

SHULE:

……

……

JINA:

……

……

1. **<u>Soma kifungu kisha ujibu swali 1-4.</u>**

   Jumatatu, Aprili 22, 2020. Saa 21:33 usiku

   Kutoka: mbogadamaris@gmail.com Kwa:

   nyakwamavyily@gmail.com

   Rafiki Willy,

   Hujambo! Unaendeleaje tangu tulipoachana siku ya uzinduzi wa upanzi wa miti? Mimi hapa Mola, amenijalia, ni buheri wa afya. Wazazi na ndugu zangu pia ni wazima, tunamshukuru Mungu.

   Sababu ya kukuandikia baruapepe hii ni kukujulisha shughuli ya upanzi wa miti katika mtaa wetu. Tulipanda takribani miche elfu kumi kwa siku saba mfululizo. Kila mkazi wa mtaa wa pendeni, wakubwa kwa wadogo, vijana kwa wazee na wake kwa waume walishiriki.

   Kama unavyofahamu, eneo la Pandeni ni kame. Mvua ilikatika ghafla, kwa hivyo, Bwana Chifu alitengeneza ratiba ya unyunyizaji maji. Siku yangu ya kunyunyizia miche maji ni Alhamisi. Je, upanzi wa miti utaanza lini kwenu? Tafadhali niarifu mapema ili niweze kushiriki. Wasalimie wote.

   Ni mimi rafiki yako,

   Mbogo Mwea.

   Hii ni aina gani ya barua?